



Tuzo ya Asasi Bora 2008

1. The Foundation for Civil Society inapenda kuwatangazia AZAKi zilizopata ruzuku kutoka kwa The Foundation for Civil Society kuanza kwa mchakato wa Tuzo ya Asasi Bora kwa mwaka 2008. Tuzo hii inatoa fursa kwa asasi za kiraia zilizopata ruzuku kutoka kwa the Foundation for Civil Society na kufanya vyema katika kutekeleza miradi hiyo. Tuzo inatoa fursa ya kutambua mafanikio, ubunifu wa asasi ambazo zimetoa mchango wa kipekee kwa kuwajengea uwezo wananchi kama njia ya kupambana na umasikini.

Malengo ya jumla ya Tuzo hii ni kuziwezesha asasi kuweza kuboresha utendaji wa kazi na kukuza taswira nzuri ya asasi za kiraia na mchango wake katika kuleta maendeleo na kuboresha ushiriki wa wananchi katika utungaji wa sera na utekelezaji na tathmini ya sera mbali mbali za maendeleo.

2. Nani Anastahili Kutuma Maombi ya Kushiriki?

- Asasi ya Kiraia ambayo imetimiza kwa ufanisi malengo ya mradi wake katika maeneo ya Sera, Utawala Bora, Mitandao ya Kiusalama (kwa makundi yaliyo hatari zaidi ya kufukarishwa) au katika eneo la Kuimarisha Utetezi miongoni mwa AZAKi.
- Asasi zinazostahili kuingia katika kinyanga'nyiro cha Asasi Bora ni zile zenye miradi iliyokuwa ikiendelea hadi Disemba 2007.

3. Maeneo ya Ushindani

- Umahiri katika utekelezaji wa masuala ya kujengea uelewa wa jamii kuhusu sera na ushiriki katika utekelezaji, uandaaji na tathmini ya sera.
- Umahiri katika utekelezaji wa miradi inayohusu utawala bora katika ngazi ya jamii au kitaifa.
- Umahiri katika miradi ya kusaidia makundi yaliyo katika hatari ya kuathirika zaidi na umasikini (Safety Nets) kama vile watu wenye ulemavu, magonjwa ya muda mrefu, watoto yatima n.k kwa kupeleka hoja zao kwa jamii na wafanya maamuzi.
- Umahiri katika kuimarisha uwezo wa ushawishi na utetezi

4. Sherehe na Utoaji Zawadi

Sherehe za utoaji zawadi kwa asasi bora zitafanyika, sanjari na Tamasha La Tano la Asasi Za Kiraia Novemba 2008. Katika kila eneo, mshindi atapata zawadi ya ngao, cheti cha ushindi, na fedha taslimu.

5. Namna ya Kuleta Maombi ya Ushiriki

Asasi zitatakiwa kujaza fomu maalumu ya maombi ya kushiriki na kuyaleta the Foundation kwa njia ya barua pepe, faksi au kwa posta katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza ikiwa na yafuatayo:

- i. Eneo ambalo shirika linaomba kushindania
- ii. Maelezo kuhusu mafanikio na mabadiliko ya mradi ulioteklezwa na ambao umefadhiliwa na the Foundation for Civil Society.
- iii. Maelezo kuhusu kiwango cha ushirikishaji wa jamii na walengwa kwenye mradi husika ili kuhakikisha uendeleu wake;
- iv. Uwezo mkubwa katika kutandaa, ujenzi wa ubia na asasi zingine za kiraia, sekta binafsi, viongozi wa serikali na viongozi wa kuchaguliwa kama madiwani na wabunge na kadhalika.
- v. Utawala Bora, uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa mradi na katika uendeshaji wa Asasi

6. Namna ya Kuingia Katika Kinyang'anyiro

Asasi zinazotaka kushiriki zitajaza fomu maalumu na kueleza eneo ambalo wanataka kushindanishwa (maeneo yametajwa katika sehemu namba tatu ya maelezo haya). Fomu hiyo iambatanishwe na yafuatayo:

- Maelezo mafupi ya ushuhuda kutoka kwa jamii au kundi lengwa la mradi (maelezo mafupi ya watu angalau wanne) waliofaidika na mradi uliofadhiliwa na the Foundation;
- Barua kutoka kwa kiongozi (wa kijiji au kata, au diwani au kiongozi yeyote wa wilaya au mkoa) ambao watasema kwa nini asasi yako inastahili kupewa ushindi katika eneo uliloomba kushindania.
- Vielelezo vingine kama picha, nakala za matukio ya utekelezaji wa miradi zilichapishwa katika magazeti na maelezo yake kuhusu mradi wenu au DVD zenye taarifa za utekelezaji za miradi yenu nk.

7. Jopo la Kupitia na Kutathmini Maombi ya Washiriki

Kila ombi la mshiriki litafanyiwa uhakiki na tathmini kulingana na maelezo yaliyotolewa katika fomu iliyoambatanishwa na maelezo yanayotajwa katika eneo la 5 na 6 la maelezo haya. Asasi ambazo zitapata alama za juu zitatembelewa na jopo la wapiga picha za video na majaji.

Majaji

Jopo la majaji wapatao 10-15 watachaguliwa kutoka miongoni mwa wabia wa maendeleo, Serikali, sekta Binafsi na Asasi za Kiraia ili kufanya uteuzi wa mwisho wa asasi bora kwa mwaka 2008.

8. Mwisho wa Kupokea Maombi

mwisho wa kupokea maombi ya ushiriki itakuwa ni tarehe 15 Septemba 2008 saa 10 jioni. Tafadhali wasilisha maombi yako kwa anuwani ifuatayo;

Tuzo ya Asasi Bora (BGA)- 2008

The Foundation for Civil Society
Haidery Plaza, ghorofa ya 5, Mtaa wa Upanga/Kisutu
SL.P 7192, Dar es Salaam, Tanzania
Faksi: +255 22 - 2138533

Barua pepe: information@thefoundation-tz.org
au: maendeleo@thefoundation-tz.org

Simu: +255 22 - 2138530 / 2138531 / 2138532
Simu ya kiganjani +255 777 – 471186, +255 713 - 486183
Tovuti: www.thefoundation-tz.org

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:
Omar Jecha

E-mail: ojecha@thefoundation-tz.org
E-mail: maendeleo@thefoundation-tz.org